Katika mwaka huu, kile kinachoharibu wengine hakitakuangamiza wewe unapobaki kuwa sawa na mapenzi ya Mungu kwa maisha yako, katika jina la Yesu.

**TAMKO LA KINABII**
Nitatoka mshindi bila kujali hali yoyote ya nyika ninayoipitia. Sitaangamizwa kwa sababu najua niko katika mapenzi ya Mungu! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 4:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 34**
Kutoka 25-26; Mathayo 20:1-19

JUMATANO, FEBRUARI 4




# USISAHAU KUHUSU KUFUNGA

**Mathayo 4:2**
**Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa.**

---

Watu wa maombi makubwa na tabia kuu ni watu wa maneno machache. Wale wanaozungumza wanataka kuonekana au kusikilizwa na kwa kawaida wanakosa maombi. Neno la kinabii linapotangazwa juu ya maisha yako, lakini udhihirisho wake ukaonekana kuchelewa, silaha moja ya kiroho ya kuitumia ni kufunga.

Kufunga husaidia kutimilika Neno lako la kinabii. Elewa kwamba kufunga hakumbadilishi Mungu, Yeye hubaki vile vile kabla, wakati na baada ya wewe kufunga. Hata hivyo, kufunga kunauvunja mwili na kukubadilisha. Ikiwa unataka mabadiliko ya kweli ya ndani, chukulia kufunga kwa uzito.

Unapofunga na kuomba katika mwezi na mwaka huu, kila Neno la kinabii linalotangazwa juu ya maisha yako litatimia kwa Jina la Yesu.

**TAMKO LA KINABII**
Nitafunga na kuomba ninapotarajia udhihirisho wa Neno langu la kinabii. Najua kufunga kunauvunja mwili wangu na kuuweka makini na kuelekeza roho yangu katika hali halisi ya ulimwengu wa roho, katika Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 17:21

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 35**
Kutoka 27-29; Mathayo 20:20-34

ALHAMISI, FEBRUARI 5



# ENDELEA KUSEMA NENO

**Yohana 11:53 (NIV)**
**Basi tangu siku ile walifanya shauri la kumwua.**

---

Ili kuelewa mstari huu, lazima uzingatie msingi na muktadha wake. Viongozi wa kidini wa siku hizo walimpinga Yesu kwa sababu walitaka kulinda vyeo vyao. Walimtesa Mtenda Miujiza ili kutunza ushawishi wao. Usishangae watu wa dini wanapokuja dhidi yako. Walifanya vivyo hivyo kwa Bwana. Kwa hivyo, ikiwa inakutokea, ujue kwamba sio jambo jipya.

Kufanya miujiza na kufanya maendeleo huvutia upinzani. Katika eneo lako la kazi, muda wa kupandishwa cheo umekaribia, afya yako, familia, au fedha zako zinaweza kushambuliwa. Adui hatawahi kupongeza maendeleo yako, anapambana nayo.

Kwa hiyo, kaa ukiwa na upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu. Endelea kutamka; endelea kusema. Tangaza kwamba umebarikiwa, na hakuna neno hasi lililotamkwa dhidi yako litakaloshinda mwaka huu.

**TAMKO LA KINABII**
Nimeketishwa pamoja na Kristo katika ulimwengu wa roho. Siwezi kushindwa, kwa kuwa Bwana atanitegemeza kwa mkono Wake wa kuume wa haki katika Jina la Yesu! Bwana asifiwe! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 22:2

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 36**
Luka 2:1-26; Zaburi 13-15

IJUMAA, FEBRUARI 6




# JIFUNZE HESHIMA

**Kutoka 20:12**
**Waheshimu baba yako na mama yako, siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako.**

---

Wengi husoma mstari huu wakifikiri tu juu ya nchi ambayo Mungu huwapa, lakini inahusisha pia wingi wa siku anazokupa. Maisha marefu yanahusiana moja kwa moja na kuheshimu baba na mama yako. (Waefeso 6:2) inathibitisha hili kwa kunukuu mstari wa leo.

Kuwaheshimu baba na mama yako kunafungua maisha marefu, ongezeko, ustawi, amani, na ulinzi wa Ki-Mungu. Hata hivyo, Wakristo wengi hufanya makosa kufikiri kwamba, kwa sababu sasa wamezaliwa mara ya pili, kuwaheshimu wazazi wao wa kimwili si lazima tena, kwamba ni wazazi wa kiroho pekee wanaohusika. Hili ni kosa kubwa. Ili kufaidika kikamilifu na ahadi hii, ni lazima uwaheshimu wazazi wako wa kimwili na wa kiroho.

Wathamini na wajali wazazi wako wakiwa bado na wewe. Kamwe usiwachukulie kuwa wa kawaida, waheshimu na uonyeshe shukrani yako kila wakati.

**TAMKO LA KINABII**
Sitawahi kujinyima baraka ya maisha marefu kwa kukosa heshima! Ustawi na amani ni vyangu ninapowaheshimu wazazi wangu wa kimwili na wa kiroho, katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 6:2

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 37**
Kutoka 30-32; Mathayo 21:1-22

**JUMAMOSI, FEBRUARI 7**




# PANDA NDANI YAKE

**Mwanzo 27:7**
**Niletee mawindo, ukanifanyie chakula kitamu ili nile, na kukubariki mbele za BWANA kabla ya kufa kwangu.**

---

Watu wengi wanatamani upako wa baba zao wa kiroho au wafanisi wao. Hata hivyo, inaweza kukushangaza kujua kwamba mara nyingi wanatarajia kupokea kiwango hicho cha upako bure! Kwa hiyo, wachache huzalisha matokeo ya kudumu katika huduma kwa sababu wengi hupuuza kanuni ya dhabihu. Ubaba wa kweli na ushirikishwaji unahitaji dhabihu.

Ikiwa unataka kukua na kumuiga mbeba neema unayoitamani, nenda zaidi ya kupendezwa naye, jiungamanishe na mbebaji kwa kupanda katika neema hiyo. Ikiwa unataka kila kitu maishani bila malipo, bila kutumikia au kupanda ndani yake, hautawahi kukithamini kwa hakika. Ndiyo maana Isaka aliomba mawindo kabla ya kuachilia baraka kwa mwanawe. Ni kanuni ya kiroho: heshima kupitia dhabihu hufungua mlango wa urithishwaji. Simamia hili maishani mwako, na utapata faida.

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni mkusanya neema. Niko tayari kupokea ushiriki kwa kumfurahisha baba yangu kwa kupanda katika maono na ajenda Mungu aliyoweka juu ya maisha yake, katika jina kuu la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 11:20

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 38**
Kutoka 33-34; Mathayo 21:23-46

JUMAPILI, FEBRUARI 8




# UWEPO DHAHILI WA MUNGU

**Yohana 11:14-15**
**Basi hapo Yesu akawaambia waziwazi, Lazaro amekufa. Nami nafurahi kwa ajili yenu kwamba sikuwako huko, ili mpate kuamini; lakini na twendeni kwake.**

---

Yesu angewezaje kifurahi ilihali Lazaro amekufa? Andiko hili linafunua kile wanatheolojia wanakiita mvutano katika maandishi, Bwana, mmiliki wa uzima, anafurahia anaposikia kifo cha mfuasi wake mpendwa. Hoja yake ilikuwa hii: Uwepo wake dhahili haukuwepo wakati Lazaro alipokufa, lakini kutokuwepo huko kulitengeneza fursa ya imani kubwa zaidi.

Wakati mwingine, mvutano wako si wa kutilia shaka nguvu za Mungu, bali ni kama atadhihirisha uwezo wake katika jambo lako. Niko hapa kukutangazia kwamba hata baada ya kwenda juu na zaidi, kustahimili kila shambulio, Yesu tayari ametuma msaada, na uko njiani. Uwepo wake hai utakutana nawe katika hatua kuu ya hitaji lako, na kila kitu kilichokufa katika maisha yako kitafufuka tena. Haleluya!

**TAMKO LA KINABII**
Nikiwa na Mungu, siwezi kushindwa! Kwa Mungu, siwezi kuguswa! Hakuna kinachoweza kunizuia kusonga mbele mwaka huu. Utukufu ni kwa Mungu! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 8:28

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 39**
Kutoka 35-37; Mathayo 22:1-22

**JUMATATU, FEBRUARI 9**




# MUONEKANO WAKE MTUKUFU

**Mathayo 24:35**
**Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe.**

---

Ninapozungumzia na kujadili unyakuo, sihubiri maangamizi au kupandikiza hofu, bali kutangaza kile ambacho Biblia inasema kitatokea katika siku za mwisho. Wengine huipuuza kama njia ya kupata ushawishi, lakini wanakosea. Wengine husema, “Hakuna mwanadamu anayejua wakati”, na hiyo inafanya ujumbe huu kuwa wa haraka zaidi.

Kuzungumzia unyakuo sio habari ya mlengo wa kimadhehebu au upandikizaji wa hofu; ni wito wa kuwa tayari kukutana na Muumba wako. Unyakuo wako binafsi unaweza kutokea wakati wowote, kwa hivyo uwe tayari kila wakati. Ishi kila siku ukiwa umevikwa haki ya Mungu.

Maneno ya Yesu ni thabiti, hayatikisiki na ni ya milele. Anachosema, anafanya. Kwa hiyo, kaa tayari, kaa imara, na kuwa macho katika mwezi na mwaka huu.

**TAMKO LA KINABII**
Niko makini, akili yangu iko tayari, moyo wangu umetayarishwa, na nitamaliza kazi yangu kwa nguvu katika Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 119:89

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 40**
Kutoka 38-40; Mathayo 22:23-46

JUMANNE, FEBRUARI 10




# JE, MUNGU NI KWA AJILI YANGU?

**Waebrania 13:8 (KJV)**
**Yesu Kristo ni yeye yule jana na leo na hata milele.**

---

Ikiwa hujawahi kuhoji kama Mungu yuko kwa ajili yako kweli, basi bado hujakabiliana na mateso makubwa. Unaweza kuwa mtu aliyejitoa zaidi, mwaminifu, mwenye akili, na mwenye bidii zaidi linapokuja suala la mambo ya Mungu lakini ukahisi kama maisha yako yanasambaratika. Kisha unaanza kujiuliza ikiwa Mungu yuko kwa ajili yako au hata anakuona.

Unahitaji kujua kwamba kuwa na Mungu katika maisha yako na kufurahia uwepo wake dhahiri ni tofauti. Tunamtumikia Mungu wa zama zote ambaye ni mvumilivu sana, na uwepo Wake hai unapofunuliwa ndani na karibu nawe, maisha yako yatakuwa na maana mpya. Uingiliaji kati wa Mungu unapodhihirika katika maisha yako, hakika utashuhudia kwamba Mungu yupo kwa ajili yako katika mwaka huu.

**TAMKO LA KINABII**
Najua Mungu wangu si msahaulifu. Niko kwenye rada Yake, kipaumbele Chake, na nimechorwa kwenye vitanga vya mikono Yake. Nimefungiwa kupiga hatua katika Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Malaki 3:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 41**
Mambo ya Walawi 1-3; Mathayo 23:1-18

JUMATANO, FEBRUARI 11



# UNATOKA NJE

**Yeremia 1:12**
**Ndipo BWANA akaniambia, Umeona vema...**

---

Mungu hajawahi kulala, kwa hivyo hana jana, na hatalala, kwa hivyo hana kesho, yuko katika umilele mmoja uitwao sasa. Kwa hivyo, Mungu anaposema, ninakubariki, inamaanisha kuwa anafanya sasa, sio baadaye.

Mara nyingi, ni mitazamo yetu inayoghairisha muujiza, kufikiri kwamba ni ya kesho, ilihali Mungu yupo tayari kufanya hivyo sasa. Hakuna kinachoweza kuzuia kiu ya Mungu juu ya usitawi wako, uponyaji, na ongezeko. Mipango yake kwa ajili ya maisha yako kamwe si ya utata, isiyoeleweka, au isiyo na uhakika. Mungu anasema katika Neno lake kwamba mipango yake kwako ni mizuri na si mibaya. Mwamini Yeye, mchukue katika Neno Lake, na utakuwa vile Mungu asemavyo wewe upo!

**TAMKO LA KINABII**
Nina hakika kwamba hakuna kina wala urefu, wasiwasi wala changamoto, malaika wala mambo yajayo yanaweza kunitenganisha na upendo wa Mungu. Ninatembea katika ushindi leo na hata milele, katika Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 55:11

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 42**
Mambo ya Walawi 4-5; Mathayo 23:19-39

ALHAMISI, FEBRUARI 12




# JARIBU NDIMI

**Yohana 2:1**
**Na siku ya tatu palikuwa na harusi huko Kana, mji wa Galilaya; naye mama yake Yesu alikuwapo.**

---

Lo, Yesu alikuwa kwenye arusi, na bado divai ikaisha! Vivyo hivyo, unaweza kuwa mhudhuriaji wa kanisa aliyeshinda tuzo nyingi zaidi au ukavaa jina la “mwanamaombi,” ilhali akaunti yako ya benki inatatizo la kuvuja damu ndani kwa ndani. Jambo kuu ni kujua jinsi ya kuamsha uwepo wa Mungu hai.

Katika ulimwengu wa roho, unaweza kuathiri wakati unaofaa wa Mungu maishani mwako kwa kuinuka katika ndimi. Unapoomba, Roho Mtakatifu hukupa msamiati unaohitajika, iwe kwa visa yako, kazi yako, kupigana na wachawi katika familia yako, au pesa zako! Lugha hufanya maombi sahihi zaidi ya ufahamu wako wa asili.

Kaa katika ndimi na ushikamane na Neno la Mungu, na utafurahia uwepo wake hai, ukimimina miujiza isiyozuilika mwaka huu.

**TAMKO LA KINABII**
Ninazungumza lugha ya Mbinguni! Ninawasilina na uungu katika ndimi zinazotikisa ufalme wa giza. Siwezi kuuwawa; atakayenigusa amekwisha! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 2:51

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 43**
Luka 2:27-52; Zaburi 16-17

IJUMAA, FEBRUARI 13



# TAFSIRI ISHARA

**Yoeli 2:1**
**Pigeni tarumbeta katika Sayuni, pigeni na kelele katika mlima wangu mtakatifu;**

---

Wakati mwingine, mahangaiko ya ghafla au uzito huja akilini mwako. Hili ni zaidi ya wazo, ni ishara kutoka ulimwengu wa kiroho, onyo kwamba kuna kitu kinakaribia kutokea. Ishara za vita hukufanya usitulie rohoni mwako.

Unapotambua ishara kama hizo, inamaanisha kuwa roho yako ipo makini na iko macho kwa mashambulizi yanayosubiri, na unahitaji kuwa tayari. Usizipuuzie; nasa ishara na kuitikia mara moja katika maombi, kufanya vita kwa Neno. Uwe macho, kwa sababu unaweza hata kuwa na Yuda aliyefichwa kwenye kambi yako.

Katika mwaka huu, kaa macho, tafsiri ishara za vita, na usimame katika ushindi.

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni askari katika jeshi la Bwana. Antena yangu ya kiroho inanasa ishara za Mbinguni kwa ajili ya vita, na kuchukua hatua. Siwezi kushtukizwa ghafla, kwa Jina la Yesu kuu! Bwana asifiwe!

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Petro 3:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 44**
Mambo ya Walawi 6-7; Mathayo 24:1-31

JUMAMOSI, FEBRUARI 14




# KAA TAYARI KWA UNYAKUO

**Mathayo 24:38**
**Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya gharika, watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina.**

---

Fikiria kwa makini msingi wa andiko ili unapochambua andiko, uweze kufahamu muktadha. Nani alikuwa anakula na kunywa? Alikuwa ni Nuhu? Hapana, alikuwa na shughuli nyingi za kujenga safina. Kula na kunywa vilikuwa kazi ya wadhambi.

Katika ulimwengu wa leo, hali hiyo hiyo inatokea, gwaride za "ufahali", sherehe za kunywa, kuimba, na aina zote za kujifurahisha kupita kiasi katika anasa za mwili. Hata hivyo, Mkristo wa kweli hukazia fikira za kuvuna nafsi na kuja kwa Bwana wetu, Yesu Kristo.

Kila jambo linalotukia sasa lilikuwa muhimili wa siku za Nuhu, lakini Noa aliendelea kuweka fokasi kwenye kazi yake aliyopewa na Mungu. Gharika ilipokuja, huku wengine wakiteseka kwa uchungu, Nuhu alikuwa na amani ya moyo.

Katika mwaka huu, usijisumbue. Kaza macho yako kwa Yesu, kwa maana kurudi kwake ni karibu zaidi kuliko unavyofikiri.

**TAMKO LA KINABII**
Ninawaka moto kwa ajili ya Yesu mpaka kuonekana kwake kwa utukufu. Niko tayari kukutana Naye mawinguni, hata sasa! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 17:26-27

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 45**
Mambo ya Walawi 8-10; Mathayo 24:32-51

JUMAPILI, FEBRUARI 15




# MKANGANYIKO!

**Mathayo 26:6**
**Naye Yesu alipokuwapo Bethania, katika nyumba ya Simoni mkoma.**

---

Yesu alikuwa katika nyumba ya Simoni mkoma. Fikiria juu ya mkanganyiko huu, Mponyaji, Mtenda Miujiza, Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yetu aliketi katika nyumba ya mtu ambaye bado anatambuliwa kwa ugonjwa wake. Maandiko hayaonyeshi rekodi ya uponyaji wa Simoni, ila tu kwamba Yesu alikuwa ameketi kwa raha katika nyumba yake. Hebu wazia kuwa mbele ya Muumba mwenyewe, lakini mwenyeji aliendelea kuwa mgonjwa.

Vivyo hivyo, unaweza kuwa mgonjwa, unateseka kupitia changamoto, au unaishi katika hali duni, lakini bado uko mbele za Mungu. Hata hivyo, ninakuhakikishia kwamba unaposoma toleo hili la Habari Njema leo, mkanganyiko huo unaisha! Kuna mpangilio mpya wa umbile la mwili wako kwa Neno la Mungu. Leo, afya yako, biashara, familia, na fedha zinarejeshwa. Hutakaa tena katika uwepo wa Mungu na kuishi maisha ya mkanganyiko!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi si mshindwa! Mimi si mtu wa kushindwa! Nitafanikiwa hata iweje, kwa maana Mungu amenipa ushindi juu sana kuliko enzi na mamlaka, katika Jina kuu la Yesu. Bwana asifiwe!

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 14:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 46**
Mambo ya Walawi 11-12; Mathayo 25:1-30

**JUMATATU, FEBRUARI 16**




# MAISHA YAKO YAKO SALAMA

**Mithali 18:10**
**Jina la BWANA ni ngome imara, Mwenye haki huikimbilia, akawa salama.**

---

Ulinzi katika Kristo ni ahadi kwa wote wanaolitumainia jina lake. (Zaburi 91:3) hutaarifu, "Maana Yeye atakuokoa na mtego wa mwindaji na katika tauni iharibuyo. Usalama wako ni muhimu kwa Kristo, na ulinzi Wake umehakikishwa kwa wale wanaomwamini. Kwa hiyo, usiogope.

Malaika wako kazini kukulinda. Unapotoka leo, hauko peke yako, unaongozwa na malaika, umezungukwa kila upande. Mungu amewekeza katika siku yako kwenda vizuri na atahakikisha hutajikwaa wala kuanguka. Hakuna ubaya utakaokupata leo. Kutoka kwako kumebarikiwa, na kuingia kwako kumebarikiwa, katika Jina la Yesu.

**TAMKO LA KINABII**
Nimebarikiwa na Bwana! Kamba yangu imeangukia mahali pazuri. Ninapotembea, shetani anaogopa sana, katika Jina kuu la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 61:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 47**
Mambo ya Walawi 13-14; Mathayo 25:31-46




# NI MARUDIO

**Mhubiri 1:9**
**Yaliyokuwako ndiyo yatakuwako, na yaliyotendeka ndiyo yaliyotendeka; wala jambo jipya hakuna chini ya jua.**

---

Kila kitu unachokiona ni marudio. Ninapotabiri kuhusu mpira wa miguu, mpira wa kikapu, au matukio mengine, kutangaza washindi na walioshindwa, ni kwa sababu tayari nimewaona katika ulimwengu wa roho. Hii inakuambia kuwa maisha jinsi unavyoyaona na kujua ni zaidi ya yanavyoonekana mwilini, ni marudio ya hali halisi ya kiroho inayojidhihirisha katika asili.

Kwa muono wa kinabii, ninatamka kuinuliwa katika biashara yako, fedha, na familia, na uponyaji katika mwili wako! Haya si maneno ya kawaida; yanabeba nguvu. Leo ni siku maalum kwako, hatima yako inainuliwa kama mnara. Udhihirisho wa miujiza katika maisha yako utakuwa wa kudumu na usio na mwisho katika mwaka huu.

**TAMKO LA KINABII**
Tayari nimebarikiwa, na haiwezi kubadilishwa. Nitaishi katika ongezeko na kibali kisichoisha katika muda wote uliosalia wa mwaka huu, katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 13:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 48**
Mambo ya Walawi 15-16; Mathayo 26:1-35




JUMATANO, FEBRUARI 18

# YESU ANARUDI PUNDE!

**1 Wakorintho 15:52**
**Kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho, maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika.**

---

Watu wengi, hata Wakristo, wanaogopa sana kutajwa kwa kunyakuliwa au kurudi kwa Kristo. Ikiwa uko tayari kwa ajili ya Mbinguni, huna cha kuogopa, tayari umeshinda! nakutangazia; hutakosa unyakuo! Ikiwa hujampokea Kristo kama Bwana na Mwokozi wako, tafuta sehemu ya “Umempokea Yesu” ya chapisho hili na uombe maombi ya kumpokea sasa!

Baragumu itakapolia ikitangaza kuja Kwake, kwa kufumba na kufumbua, utanyakuliwa ili kukutana na Bwana mawinguni. Kwa hiyo, acha kuhangaika na uanze kufurahi. Jizoeze kuishi katika hali ya “unyakuo wa kwanza”, tayari kila wakati kwa ujio Wake. Katika mwaka huu utakuwemo katika hesabu!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni wa Mbinguni na niko tayari kwa unyakuo! Adui hawezi kunishawishi kuacha. Mimi nina nia ya Ufalme na sitaachwa nyuma kamwe. Bwana asifiwe! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 24:31

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 49**
Mambo ya Walawi 17-19; Mathayo 26:36-75

**ALHAMISI, FEBRUARI 19**




# UPONYWE

**Mathayo 15:30**
**Wakamwendea makutano mengi wakimletea viwete, vipofu, viwete, mabubu,vilema, na wengine wengi, Wakawaweka miguuni pake, akawaponya.**

---

Kuna miujiza ya kushangaza ambayo watu wanashangaa, hatujawahi kuona ikifanywa kwa mtindo huu! Katika kutembea kwangu na Mungu, nimeshuhudia uponyaji usiohesabika, lakini ninashangazwa na idadi ya wagonjwa wa VVU kuponywa. Iwe ni katika makongamano au ibada za Jumapili, VVU hujitokeza mara moja tunapotangaza uponyaji katika Jina la Yesu.

Haijalishi ni ugonjwa gani au hali gani ya kiafya, Yesu yule yule ambaye ameponya magonjwa magumu mara kwa mara analeta uponyaji katika mwili wako sasa hivi! Pokea! Mifupa yako, mishipa ya damu, na viungo vinarejeshwa. Yesu Mponyaji anaugusa mwili wako unaposoma Habari Njema Kila Siku kwa imani. Amini tu, na uponyaji wako utadhihirika katika jina kuu la Yesu!

**TAMKO LA KINABII**
Sitapambana na homa au magonjwa. Mwili wangu unakataa kila udhaifu. Ninaishi katika afya kamilifu, katika Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 6:2

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 50**
Luka 3:1-19; Zaburi 18-19

IJUMAA, FEBRUARI 20




# YOTE NI YESU

**Yohana 14:14**
**Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.**

---

Katika uwanja uliojaa watu wengi katika eneo la Copperbelt nchini Zambia, wakati wa Kongamano la Habari Njema mnamo Agosti 2025, nilijionea nguvu za kimuujiza za Mungu. Sikuhubiri kwa ufasaha wa kibinadamu bali kwa udhihirisho wa nguvu, kama inavyotangazwa katika (1 Wakorintho 2:4). Makumi ya maelfu katika uwanja wa michezo na mamilioni ya watu ulimwenguni pote walimwona Yesu akifanya kazi!

Kupooza kuliponywa, VVU ilitoweka, pesa za miujiza zilionekana kwenye simu za mkononi na hata pesa taslimu. Vifaa vilivyoharibika, kama vile skrini za simu zilizopasuka, zilirekebishwa kwa njia isiyo ya kawaida bila chembe ya uharibifu wa hapo awali. Hali za damu kama VVU ziliponywa tena na tena. Inaweza kuwa Yesu pekee!

Madaktari hutumia sharubati, vidonge na sindano ili kupunguza dalili za ugonjwa, lakini Neno moja kutoka kwa Mungu huleta miujiza, ishara na maajabu ya papo hapo, bila athari mbaya. Inaweza kuwa YESU pekee!

**TAMKO LA KINABII**
Inaweza tu kuwa Yesu ananiongoza kufanya mambo makubwa katika mwaka huu haswa. Siwezi kuzuiliwa au kukata tamaa, kwa maana Yeye huniongoza kutoka utukufu hadi utukufu! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 3:22

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 51**
Mambo ya Walawi 20-22; Mathayo 27:1-32

JUMAMOSI, FEBRUARI 21



# NJAA YA MUNGU

**Mwanzo 5:24**
**Henoko akaenda pamoja na Mungu, naye akatoweka; maana Mungu alimtwaa.**

---

Wakristo wengi wanatafuta nguvu, sifa, au kutambuliwa, lakini njaa yao ya mambo ya Mungu ni ndogo. Nimekutana na watu wanaotamani udhihirisho lakini hawana njaa ya urafiki wa kweli na Mungu wa Mbinguni. Wanataka "vitu" vyake lakini wamefilisika katika upendo wake.

Mwanamume au mwanamke aliye na njaa isiyoweza kuisha kwa Mungu anaamuru nguvu na kubadilisha hatima. Ni wakati wa wewe kuwa mtu huyo, mtu ambaye anawaka na hamu isiyokwisha na isiyoweza kuzimika kwa ajili Yake. Katika mwaka huu acha njaa yako ipande hadi kufikia kiwango ambacho Mungu anaweza kukukabidhi uwezo wa kuleta mabadiliko katika familia yako, biashara, kazi, na fedha bila shida.

**TAMKO LA KINABII**
Njaa yangu kwa Mungu haijachakachuliwa! Hamu yangu Kwake inapokua, natiwa nguvu na kuingia kwa ujasiri katika uhalisi wa Roho. Maisha yangu yanainuka katika utukufu, katika Jina la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 24:51

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 52**
Mambo ya Walawi 23-25; Mathayo 27:33-66

JUMAPILI, FEBRUARI 22




# FOKASI YA KIMAOMBI

**1 Wafalme 18:42**
**Basi Ahabu akainuka ili kula na kunywa. Naye Eliya akapanda juu mpaka kilele cha Karmeli; akasujudu kifudifudi, akainama uso wake mpaka magotini.**

---

Nabii Eliya aliomba huku uso wake ukiwa katikati ya magoti yake. Kichwa chake, ambacho kina macho, masikio, mdomo, pua na ubongo, kiliinama kwa utii kamili. Mkao huu ulionyesha kwamba kila kitivo chake kilikuwa kikishiriki katika maombi makali, bila kuacha nafasi ya kukengeushwa.

Ni katika hatua ya mkusanyiko kamili ambapo moto kutoka kwenye chumba cha enzi hupenya kila upinzani kwa maendeleo yako. Acha wakati wako katika maombi uwe wa fokasi kamili, umakini kamili unaofumbatwa katika imani na matarajio, na matokeo hakika yatadhihirika. Maombi kama haya hutekeleza ukweli wa mbinguni na miujiza ya kuzaliwa. Fanya hivi kwa makusudi, na maisha yako yatapaa mwaka huu.

**TAMKO LA KINABII**
Ninaomba na kuzaa matokeo! Mambi yangu hutikisa himaya na kulazimisha hali zishindwe na Neno la Mungu lililo ndani yangu. Maombi yangu yanalenga matokeo kwa sababu ninafokasi katika kuendeleza ajenda ya Mungu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yakobo 5:17-18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 53**
Mambo ya Walawi 26-27; Mathayo 28

**JUMATATU, FEBRUARI 23**




# WAKATI WA KUJITENGA

**1 Wafalme 19:9**
**Akafika kunako pango, akalala ndani yake. Na tazama, neno la BWANA likamjia, naye akamwambia, Unafanya nini hapa, Eliya?**

---

Kuna nyakati na majira ya kuwa miongoni mwa umati, kupiga kelele, kuimba, na kusherehekea. Pia kuna nyakati muhimu ambapo mabadiliko ya maisha yanadai kujitenga. Ni katika nyakati za upweke ndipo Mungu anaanza kuzungumza nawe.
Eliya, nabii mashuhuri, alisafiri mbali na kulala katika pango, mbali kabisa na kusanyiko. Hapo ndipo Neno la Bwana lilimjia.

Umekaa katika mazingira yenye kelele kwa muda mrefu sana, ukichanganyika na umati ili kupata maumivu yaliyorejeshwa, kufadhaika na kukatishwa tamaa. Lakini unapothubutu kujitenga kwa ujasiri kutoka kwenye kusanyiko katika mwaka huu, Mungu atakutana nawe kwa kutaniko la Ki-Ungu ambalo linabadilisha hatima yako milele.

**TAMKO LA KINABII**
Sitapata usingizi machoni mwangu mpaka Mungu aseme wakati wa kujitenga kwangu. Ninajua Mungu anazungumza, na niko katika nafasi nzuri ya kumsikia kwa uwazi, katika Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 46:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 54**
Hesabu 1-2; Marko 1:1-22



# NAFASI YA MOYO

**Yeremia 17:9**
**Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; Nani awezae kuujua?**

---

Tunaishi katika ulimwengu ambamo watu wengi hujitahidi kuwavutia wengine. Wengine hutabasamu, hucheka, na huonekana kuwa wenye furaha, lakini hali halisi ya moyo ikoje?

Katika moja ya huduma zetu, wanandoa waliingia wakitabasamu, wakiwa wameshikana mikono, wakivutia wote. Kwa macho ya kawaida, upendo wao ulionekana kama umeundwa Mbinguni. Lakini unabii ulipotoka, ilifunuliwa kwamba walikuwa kwenye hatihati ya kutalikiana. Kwa kushangaza, mke alikuwa tayari amefungua shauri la talaka, lakini mwanamume hakuwa na habari kabisa. Uthibitisho wa mke kwa Neno la kinabii ulimwacha mume akiwa amepigwa na butwaa.

Mungu hahukumu kwa sura ya nje, bali kwa jinsi moyo ulivyo. Hebu aone kwamba moyo wako umewekwa wakfu Kwake katika mwaka huu.

**TAMKO LA KINABII**
Moyo wangu unakubali Neno la Mungu. Roho yangu inajilingana na maagizo yake. Kwa hiyo, ninaweza tu kusonga juu zaidi, katika Jina la Yesu! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Waebrania 4:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 55**
Hesabu 3-4; Marko 1:23-45

JUMATANO, FEBRUARI 25



# BUSTA YA ROKETI

**1 Yohana 2:19**
**Walitoka kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu. Maana kama wangalikuwa wa kwetu, wangalikaa pamoja nasi…**

---

Busta ya roketi hutoa msukumo unaohitajika ili roketi inyanyuke, lakini roketi inapofika umbali fulani, busta hujiondoa na kuiacha iendelee na mzunguko wake.

Vivyo hivyo, watu wengine wamekusudiwa tu kuandamana nawe kwa sehemu fulani ya safari yako. Hata hivyo Wakristo wengi hupoteza usingizi wakishangaa kwa nini mtu fulani alichagua kuondoka, licha ya yote waliyowafanyia. Ukweli ni watu fulani na vitu haviwezi kukusindikiza kwenye hatua yako inayofuata.

Ni wakati wa kukubali mawazo ya mwanasayansi wa roketi: tazama kuondoka kwao kama muhimu kwa mwinuko wako. Katika mwaka huu lipuka, viache viende vile visivyoweza kubaki nawe, kisha upae!

**TAMKO LA KINABII**
Nimezaliwa mshindi! Siwezi kushindwa, pamoja na au bila "wao." Nimejitayarisha kwa ushindi na nitaonyesha utukufu wa Mungu sasa na siku zote, katika Jina kuu la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Timotheo 4:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 56**
Hesabu 5-6; Marko 2:1-28



# IMEKWISHA!

**Yohana 19:30**
**Basi Yesu alipokwisha kuipokea ile siki, alisema, Imekwisha.**

---

Yesu alipotangaza kwa ujasiri, "IMEKWISHA!" kwa wale walio karibu Naye na viumbe kwa ujumla wake, ilikuwa ni kauli iliyorejea katika umilele. Dhambi zako zilizopita, za sasa na zijazo zote zilishughulikiwa juu ya msalaba huo. Yesu hayuko katika biashara ya kupatiliza makosa yako, kwa hiyo usijisulubishe mwenyewe!

Damu yake iliyomwagwa ilikuwa malipo kamili ya dhambi ya wanadamu. Kujua kwamba Alilipa gharama kuu kunapaswa kujaza moyo wako na furaha na amani, si hatia au hukumu. Yesu anaposema imekwisha, ina maana kwamba jambo hilo limetatuliwa, huna haja ya kuwa na wasiwasi juu yake tena. Umesamehewa, na rekodi ya makosa imefutwa kabisa.

Sherehekea uhuru wako leo kwa shukrani, kwa kuwa katika Kristo wewe ni huru kweli!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo! Maisha yangu sasa yamefichwa ndani Yake. Mimi niko vile Mungu anasema niko, na niko tayari kushawishi mataifa kwa ajili ya Kristo! Bwana asifiwe! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 5:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 57**
Luka 3:20-38; Zaburi 20-22

IJUMAA, FEBRUARI 27




# WACHA NURU YAKO ING'AE!

**Luka 8:16**
**Hakuna mtu ambaye akiisha kuiwasha taa huifunika kwa chombo, au kuiweka mvunguni; bali huiweka juu ya kiango, ili waingiao wapate kuona nuru yake.**

---

Uamsho ni kuamka kutoka kwa ubaridi wa kiroho na usingizi na kuingia katika hali halisi mpya katika Kristo. Maandiko yanasema hakuna mtu anayewasha taa na kuificha. Yesu anapokuita nuru ya ulimwengu maana yake unatawanya giza, hulivutii.

Mwanga uliobeba ni phótizó , mwanga wa uwanja unang'aa sana hivyo humpofusha adui. Pia ni moto unaotoka kwa Roho Mtakatifu ndani yako. Umeitwa kuangaza mazingira yako. Kwa hivyo, usiruhusu giza kushika ndoa yako, familia, biashara, au kazi yako. Inuka, uangaze! Kwa maana nuru yako imekuja.

**TAMKO LA KINABII**
Ninaangaza kama taa ya uwanja! Ninainuka kama mnara. Giza halina mahali pa kujificha mahali pangu. Ninabeba nguvu za Mungu na moto wa Roho Mtakatifu ndani yangu. Haleluya! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 4:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 58**
Hesabu 7-8; Marko 3:1-19

JUMAMOSI, FEBRUARI 28



# MANUFAA MUHIMU YA KU-HESHIMU

**Waefeso 6:2**
**Waheshimu baba yako na mama yako; amri hii ndiyo amri ya kwan-za yenye ahadi.**

---

Kuna baraka zinazoambatanishwa na kuheshimu baba na mama, iwe ya kimwili au wa kiroho. Ni muhimu kuliweka hili sawa. Kwa kuwaheshimu wazazi wako, unapata maisha marefu, kubatilishwa kwa hukumu za kifo, ulinzi dhidi ya ajali, na hukumu ya "kutokuwa na hatia" kutokana na shutuma za adui ambazo angejaribu kutumia ili kukuondoa.

Heshima si dhana dhahania ya kiroho; inadhihirishwa kimwili. Usingoje kukumbushwa kuwathamini na kuwaheshimu wazazi wako wa kukuzaa na wale wanaokuzaa katika Bwana. Heshima ni kanuni ya kiroho inayovuta baraka za Mungu. Pia ni amri inayokuja na ahadi: ili siku zako zipate kuwa nyingi duniani.

Katika mwaka huu, unapowaheshimu wazazi wa kimwili na wa kiroho, maisha marefu na kutunzwa Ki-Ungu ni kwako.

**TAMKO LA KINABII**
Nitawaheshimu wazazi wangu wa kimwili na wa kiroho kwa maneno na vitendo. Niko tayari kupokea faida kamili za kuheshimu sasa na siku zote! Haleluya! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Kutoka 20:12

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 59**
Hesabu 9-10; Marko 3:20-35

JUMAPILI, MACHI 1




# FAIDA ISIYONG'AMULIWA

**Mathayo 7:24**
**Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba.**

---

Katika ulimwengu wa uwekezaji, wajasiriamali wengi wanaelewa dhana ya "faida isiyong'amuliwa", faida ambayo iliyo kwenye makaratasi lakini haijatekelezwa kwa sababu mali haijauzwa. Hebu fikiria kununua hisa kwa $1000, ambayo baadaye itapanda hadi $1500. Ongezeko hilo la $500 ni faida yako isiyoweza kuonekana ambayo inakuwa halisi tu unapouza hisa.

Kwa Wakristo, kushindwa kuamsha maandiko kunamaanisha kuhatarisha maisha ya faida isiyong'amuliwa, kutopata kamwe thawabu ambazo Mungu amehifadhi. Neno linakuwa faida ya karatasi, iliyojaa ahadi za Ki-Mungu ambazo hubakia palepale. Mstari juu ya mstari, amri juu ya kanuni, maandiko yanaeleza mpango wa Mungu kwa ajili ya kukua kwako, lakini bila matendo, haufanyi kazi yoyote. Lifanyie kazi Neno, usilisikie tu, lifanye!

**TAMKO LA KINABII**
Leo sichagui tu kusikiliza Neno bali kulifanyia kazi! Ninaamsha kila upaji wa Ki-Ungu ulioandikwa kunihusu. Sitaishi na faida isiyong'amuliwa; Ninadai yote ambayo Mungu ametangaza juu ya maisha yangu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Yakobo 1:22

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 60**
Hesabu 11-13; Marko 4:1-20



JUMATATU, MACHI 2

# MACHO YA MUNGU

**Waamuzi 6:15**
**Akamwambia, Ee Bwana, nitawaokoa Israeli kwa jinsi gani?**

---

Katika andiko la leo, Mungu anamwita Gideoni wakati ambapo Waisraeli walikandamizwa na Wamidiani. Bwana alisema, “Nenda kwa uwezo wako huu, nawe utawaokoa Israeli na mikono ya Wamidiani…” Kinachofanya maandiko haya kuwa na matokeo ni jibu la Gideoni. Badala ya kutembea kwa uhakika katika jinsi Mungu alivyomwita kuwa, aliitikia kwa woga, akijipima uwezo wake kupitia macho ya wanadamu.

Wakristo wengi leo hufanya vivyo hivyo, wakikwamisha mtembeo wa Mungu maishani mwao kwa kudharau nafasi ya wao ni nani ndani ya Kristo. Wanahisi kutostahili, dhaifu, au wadogo sana. Lakini haijalishi ikiwa wengine wanakuchukulia kuwa mdogo zaidi katika nafasi yako ya elimu, mahali pa kazi, au jumuiya; ikiwa Mungu amekuita, atakutia nguvu. Utatimiza utume wake kwa namna kuu!

**TAMKO LA KINABII**
Leo, ninachagua kujitazama kupitia lenzi ya macho ya Mungu. Ninatembea kwa ujasiri katika wiki mpya nikijua nimechaguliwa na Mungu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Yeremia 1:5-8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 61**
Hesabu 14-15; Marko 4:21-41



# USTADI WA TAI

**Wafilipi 3:14**
**nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu.**

Katika ornitholojia (elimu juu ya ndege), tai huchukuliwa kati ya viumbe vyenye fokasi zaidi, vya kimkakati, na makini katika kundi la wanyama. Kwa uwezo wa kuona mara nane kuliko binadamu, wanaweza kuona mawindo kutoka umbali wa maili, hata kwa urefu wa futi 23,000. Zaidi ya uwezo wao wa kimwili, tai wana mawazo tofauti na ya viumbe wengine wanaoruka; hawana kuchoka katika kutafuta mawindo yao. Bila kushtushwa na kutotikisika.

Kama mtoto wa Mungu, tekeleza kila kazi kwa usahihi wa tai. Usichoke katika harakati zako za kutekeleza mapenzi ya Mungu, kwa umakini na mkakati wa makali ya wembe. Kaza macho yako daima katika kutimiza mpango wa Mungu na kuendeleza ajenda ya Ufalme wake, huku ukikaza mwendo kuelekea alama ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu!

**TAMKO LA KINABII**
Kama tai, nimefanywa kupaa! Nina kila chombo ninachoniwezesha kutekeleza mapenzi ya Mungu kwa maisha yangu kwa usahihi na kimkakati!

**MAFUNZO ZAIDI**
Wakolosai 3:2

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 62**
Numbers 14-15; Marko 4:21-41

**JUMATANO, MACHI 4**




# SITAKUWA TANKI TUPU

**Warumi 12:11**
**Kwa bidii, si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana.**

---

Wakristo wengi wanaishi maisha yao ya kila siku bila kupata faida zote ambazo Kristo alitupa kupitia kifo chake na ufufuo wa utukufu, kwa sababu tu wametulia katika hisia potofu ya maendeleo ya kiroho. Wanaacha kutafuta kusoma Neno kwa kina zaidi, viwango vya juu vya maombi, na kujitoa kwa umakini kwenye Ufalme; wamekuwa wa kuridhika.

Fikiria kuendesha gari lililojazwa mafuta robo ya tanki. Hakika, sio ya kukatisha tamaa kama kuwa tupu kabisa, lakini bado iko mbali na tanki lililojaa! Kama mtoto wa Mungu, usichanganye “kuwa bora kuliko hapo awali” na kuwa mahali ambapo Mungu amekukusudia. Usikubali kuishi chini ya kiwango ambacho Mungu amekuwekea. Maendeleo ya kweli hayahusu kuwa bora kuliko mabaya yako bali kusonga mbele kuelekea bora zaidi kwa Kristo kwenye maisha yako!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi sitaridhika na uafadhali; Ninafuata yaliyo bora ya Mungu kwangu! Siwezi kamwe kuwa mwenye tanki tupu. Nimejaa nguvu za Kimungu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 3:19

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 63**
Hesabu 19-20; Marko 5:22-43

ALHAMISI, MACHI 5




# “HAKUNA ALIYE MKAMILIFU”

**Mathayo 5:48**
**Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.**

---

Kuna udanganyifu ambao adui anaukuza ambao umepenya mioyo ya mamilioni ya watu: ni maneno “hakuna aliye mkamilifu.” Ingawa inaweza kuonekana kuwa ya unyenyekevu na ya vitendo, inapingana na ukweli uliofunuliwa katika maandiko. Ukiuruhusu kuyaongoza maisha yako, madhara yanaweza kuwa mabaya.

Ndiyo, mwanadamu ana kasoro, lakini unapomkubali Kristo, unapokea asili Yake na unaitwa kuishi kwa kiwango chake cha mbinguni, si mifumo ya mwanadamu wa kimwili. Mungu alitupa Roho Mtakatifu na karama za Roho kwa ajili ya kuwakamilisha watakatifu, hiyo inamaanisha wewe!

Yesu, kielelezo chetu kisicho na dosari, anaonyesha kwamba ukamilifu ni kuishi kupatana na mapenzi ya Mungu, kurekebisha maisha yako kwa haki yake. Ukristo halisi ni udhihirisho wa ukweli, ishi katika ukweli huu leo!

**TAMKO LA KINABII**
Mungu amenipa maisha makamilifu! Ninaishi kulingana na kiwango chake cha mbinguni. Ninakataa utamaduni usiokamilika wa dunia hii leo; Ninaishi kwa kupatana na mapenzi Yake!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 4:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 64**
Luka 4:1-22; Zaburi 23-25

IJUMAA, MACHI 6




# UHUSIANO NA UUNGU

**Yakobo 4:8**
**Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi; na kuisafisha mioyo yenu, enyi wenye nia mbili.**

---

Kinachotofautisha Ukristo na dini zingine ni kwamba ukristo sio dini kwa maana ya kiutamaduni; ni uhusiano na Uungu! Mungu alitupenda sana hata akachagua kukaa kati yetu, kuchukua adhabu yetu kwa njia ya msalaba, na kutukomboa kwa ufufuo wake wa utukufu. Yeye ni Mungu mwenye utu ambaye anakupenda kupita ufahamu wa kibinadamu na anataka uishi maisha ya urembo katika Kristo.

Maandiko yanafunua kwamba unapomkaribia Mungu, Yeye anakukaribia zaidi. Kwa kuzama ndani ya Neno Lake, unawekeza wakati wa thamani katika kuimarisha uhusiano huu wa Ki-Ungu na, kwa matokeo yake, kufungua madirisha ya baraka na fursa nyingi zisizohesabika.

Kama uhusiano wowote, mawasiliano ni muhimu. Zungumza Naye kuhusu mambo unayopenda, changamoto, kila kitu, kwa sababu Yeye anakujali kikweli.

**TAMKO LA KINABII**
Nina uhusiano na Mungu anayenijali! Ninapomkaribia Yeye kila siku, ninabadilishwa na kuwezeshwa kutekeleza mapenzi Yake. Ninatembea katika ukaribu wa Ki-Ungu na amani kamilifu katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 145:18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 65**
Hesabu 21-22; Marko 6:1-31




# MATAMANIO HUKAMILISHA KUSUDI

**Wakolosai 3:23**
**Lolote mfanyalo, lifanyeni kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa wanadamu.**

---

Kuna maoni potofu ya kawaida kwamba kusudi la Mungu kwenye maisha yako linapingana na matarajio yako na kwamba ili kutekeleza mapenzi yake, lazima uachane na tamaa zako. Walakini, hii haiwezi kuwa mbali na ukweli! Maandiko yanafundisha kwamba Mungu hutufanya tupende na kutenda kulingana na kusudi Lake jema. Unapopatana na mapenzi Yake, matamanio yako si ya ubinafsi; yana makusudi.

Kwa mfano, ikiwa nia yako ni kuwa bora katika sekta ya hospitali ya anasa na kusudi lako ulilopewa na Mungu ni kuinjilisha, faida yako ya biashara inaweza kufadhili misheni, huduma ya usaidizi, na kuunda fursa za kushiriki Injili. Mungu anataka ufanikiwe. Maadamu matamanio yako hayazuii mwito wa Mungu maishani mwako bali yanakamilisha, yanakuwa zana zenye nguvu kwa utukufu Wake.

**TAMKO LA KINABII**
Mungu amenipa msukumo wa kufanya matendo mema! Iwe katika huduma au sekta ya biashara, mafanikio yangu ni hakika kama jua linapochomoza asubuhi!

**MAFUNZO ZAIDI**
Philippians 2:13

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 66**
Hesabu 23-25; Marko 6:32-56




# MBEBA HABARI MBAYA

**1 Petro 5:7**
**huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.**

---

Usahihi wa Neno la Mungu unaonekana katika usahihi wa kudumu wa kihistoria na umuhimu wa maisha halisi. Lakini Wakristo wengi bado wanahisi kulemewa na maisha, licha ya Maandiko kutuhakikishia amani kutoka kwa Mungu. Amani hii inagawiwa kwa kila mtoto wa Mungu anapopokea uzima na Roho wake. Hili halifichui dosari katika Neno la Mungu, bali ni tatizo katika Kanisa la kisasa.

Mamilioni ya Wakristo wanaishi katika hali ya uchovu na kutotulia, si kwa sababu wao ni dhaifu, lakini kwa sababu wanabeba mizigo ambayo hawakupaswa kubeba. Badala ya kumtwika Yesu mahangaiko yao, wanayashikilia. Hujaitwa kuwa mbeba habari mbaya. Unachotakiwa kufanya ni kutembea katika amani kamilifu na ushindi ambao Kristo tayari amekuwekea.

**TAMKO LA KINABII**
Mimi sio mbeba habari mbaya! Si juu yangu kubeba uzito wa hali ambazo ninaweza kukabiliana nazo. Ninamtumikia Mungu ambaye ameniwekea njia ya ushindi, nami nitatembea ndani yake!

**MAFUNZO ZAIDI**
Philippians 4:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 67**
Numbers 23-25; Marko 6:32-56

JUMATATU, MACHI 9




# MAOMBI YA KUTOKA MOYONI

**Marko 11:24**
**Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.**

---

Unyoofu wa maombi haupimwi kwa usemi fasaha au ladha ya kishairi. Kilicho muhimu zaidi kwa Mungu ni hali ya moyo wako. Imani imekita mizizi ndani ya moyo. Maandiko yanatuambia, "Kwa moyo mtu huamini hata kupata haki." Imani ni wonyesho wa nje wa kuamini kwetu katika Neno la Mungu. Unapodhihirisha imani yako kupitia maneno, inakuwa dhihirisho la imani iliyo moyoni mwako.

Wakristo wengi wanadhani maombi yao hayajibiwi kwa sababu wamekosa ukweli huu. Hata hivyo, elewa kwamba kukiri kwako katika maombi ni zaidi ya kurudia tu yale ambayo Mungu amesema kukuhusu; ni kunena kwa kukubaliana na imani yako katika kupatana na Neno la Mungu. Sala ya kutoka moyoni ina uwezo wa kubadilisha kabisa maisha yako na kukufungulia yaliyo bora zaidi ya Kristo. Shika nguvu hiyo leo!

**TAMKO LA KINABII**
Ninaposali, moyo wangu unapatana na yale ambayo Maandiko yanasema kunihusu! Kupitia maombi ya dhati, ninabadilishwa na ninaunda njia iliyo wazi ya mafanikio maishani mwangu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 10:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 68**
Hesabu 28-30; Marko 7:24-37




# DOZI YA ROHO MTAKATIFU

**Waefeso 5:18**
**Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho.**

---

Inaweza kukushtua kujua kwamba hisia ambazo watu huzipata kupitia pombe, dawa za kulevya, au vitu vingine sawa na hivyo vinahusisha viungo vilevile vya mwili ambavyo Roho Mtakatifu huvigusa unapo "lewa katika Roho." Siku ya Pentekoste, wakati Roho Mtakatifu alipomiminwa, watazamaji waliwadhihaki wanafunzi, wakisema maneno kama "hawa lazima wamelewa," bila kutambua furaha na shangwe kama hiyo ingeweza kupatikana tu kupitia ushirika na Roho Mtakatifu!

Unapojazwa na Roho, ni kama mikondo ya umeme inatiririka kupitia mifupa yako, damu, uwazi katika mifupa na mwili, ikihuisha na kuimarisha kila sehemu yako! Unapokuwa na Kristo, hakuna haja ya mbadala; dozi ya kitu kingine chochote haiwezi kuwa mbadala. Jiepushe na tamaa za kimwili na vikengeusha-fikira, elekeza macho yako juu, na ujazwe na Roho Wake!

**TAMKO LA KINABII**
Roho Mtakatifu ndani yangu ni kama mikondo ya umeme inayopita katika mwili wangu! Ninapojiweka wazi na kumruhusu achukue udhibiti, ninaimarishwa na kujiandaa kukabiliana na changamoto yoyote!

**MAFUNZO ZAIDI**
Matendo 1:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 69**
Hesabu 31-32; Marko 8:1-21




# WARITHI DHAHIRI

**Wagalatia 4:1**
**Lakini nasema ya kuwa mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, ingawa ni bwana wa yote.**

---

Hapo zamani za kale, wafalme mashuhuri na nasaba mashuhuri ziliwawekea wazao wao urithi, wakihakikisha kwamba utajiri na urithi wao unaendelea. Wale walio na haki ya kurithi lakini bado kusimikwa waliitwa warithi dhahiri. Kwa kusikitisha, Wakristo wengi wanaishi maisha yao yote bila kudai urithi wao kamili wa Ki-Mungu. Kwa nini? Kwa sababu wanahangaika kuacha anasa za dunia na kujisalimisha kwa Mungu.

Katika historia yote, warithi dhahiri mara nyingi walikuwa watu wachanga, ndiyo maana Biblia inawafafanua wale waliofungwa na tamaa za kimwili kuwa watoto! Mradi tu unang'ang'ania anasa za muda mfupi za ulimwengu huu, utaishi kama mtoto, chini ya kiwango cha stahiki zako ya Ki-Ungu. Ukomavu wa kweli huanza pale unapokumbatia urithi wako kamili katika Kristo!

**TAMKO LA KINABII**
Urithi ambao Kristo aliniriithisha ni wa thamani zaidi kuliko mali au umaarufu. Mungu ameniweka kwa mafanikio! Ninakataa ulimwengu na kuchukua nafasi yangu kati ya wasio wa kawaida. Ukata haujui anwani yangu, kwa Jina kuu la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Wagalatia 4:3

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 70**
Hesabu 33-34; Marko 8:22-38



# OMBAOMBA HAWAWEZI KUWA WACHAGUZI

**Ufunuo 1:6**
**Na kutufanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una yeye hata milele na milele. Amina.**

---

Mungu amewafanya watoto wake kuwa wafalme na makuhani! Sehemu muhimu ya mafunzo yako ni kuelewa kanuni hii rahisi lakini muhimu: wafalme hawaombi ! Huenda umesikia maneno haya, "ombaomba hawawezi kuwa wachaguzi." Kwa maneno mengine, ikiwa unajiweka kama ombaomba, kila wakati ukiwa unaridhika kupata kidogo, unakuwa chini ya hali na kusalimisha uwezo wa kuchagua matokeo bora ya Mungu.

Mungu amekupa uwezo wa kutiisha kila hali.

Ukiwa mzao wa Mungu, umeitwa kujibeba kwa namna inayoakisi mamlaka, neema, na wingi ufaao wa kifalme. Ingawa kuishi kama ulimwengu kunaweza kumtosha mwanadamu wa kimwili, wito wa Mungu kwako ni wa juu zaidi. Tembea kama mfalme, sio ombaomba!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni wa KIFALME! Ulimwengu na mifumo yake ni watendaji wangu. Siwezi kamwe kukosa au kuwa na huzuni. Sihitaji kumwomba Mungu afanye mabadiliko katika maisha yangu; Tayari amefanya hivyo. Ushindi ni wangu!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 2:9

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 71**
Luka 4:23-44; Zaburi 26-28

IJUMAA, MACHI 13




# USTAWI THABITI

**2 Wakorintho 8:9**
**Maana mmejua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu, ingawa alikuwa tajiri, ili ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake.**

---

Hakuna nafasi ya umaskini katika Ukristo! Ingawa hii inaweza kuonekana kuwa kauli ya uchochezi au yenye utata, maandiko yanathibitisha ukweli huu wa kiroho na kimwili. Watoto wa Mungu hawako chini ya mifumo ya ulimwengu. Kwa hakika, tumeitwa kuuweka juu ufalme wetu wa mbinguni kwa ustawi kamili na wingi juu yake.

Unaweza kuchagua umaskini kwa kupuuza yote ambayo Kristo aliyakomboa kupitia kifo na ufufuo Wake, kuishi chini ya utambulisho wako wa Ki-Ungu, au unaweza kuchagua kutembea katika wingi kamili wa kila ahadi Aliyotimiza. Urithi wako katika Bwana ni maisha ambayo ukosefu, magonjwa, na mabaya hayawezi kukupata kamwe, maisha ya MAFANIKIO THABITI!

**TAMKO LA KINABII**
Ninafanikiwa katika kila kitu ninachofanya! Ninakataa maisha ya umaskini, yanayowakilisha vibaya karama ambazo Kristo aliweka kwa ajili yangu. Utajiri wangu na kustawi kwangu havina mipaka. Madirisha ya fursa na baraka yatanipata mwaka huu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 10:10

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 72**
Hesabu 35-36; Marko 9:1-32

JUMAMOSI, MACHI 14




# MGAWA UPENDO

**1 Yohana 4:20**
**Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; Kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona.**

---

Je, haishangazi ni wangapi wanaodai kumpenda Bwana kwa moyo wao wote na roho zao zote? Lakini upendo huo unabaki bila kuthibitishwa ikiwa hauonyeshwi kwa wale wanaoweza kuuona. Maandiko yako wazi, ukiwa na chuki hata kwa mtu mmoja, madai yako ya kumpenda Mungu ni uongo! Ni rahisi kukiri kujitoa kwa Kristo, lakini upendo wa kweli unadhihirishwa katika jinsi unavyowatendea wengine.

Wengi wanashangaa kwa nini hawajawahi kupata baraka katika Maandiko, bila kutambua kwamba machoni pa Mungu, hawahesabiwi miongoni mwa wale wanaompenda Yeye kweli. Kwa nini? Kwa sababu ya chuki waliyo nayo mioyoni mwao kwa jirani zao. Wapende hata wasiopendeka kabisa, si kwa sababu wanastahili, bali kwa sababu Kristo alikupenda kwanza, hata katika hali yako mbaya zaidi.

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni mgawa upendo! Upendo wangu kwa wengine ni uthibitisho wa Mungu ni nani kwangu. Chuki, uchoyo na uchungu hauwezi kamwe kupatikana ndani yangu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 5:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 73**
Kumbukumbu la Torati 1-3; Marko 9:33-50

JUMAPILI, MACHI 15




# HATIA KAMA ANAVYOSHITAKIWA

**Nahumu 1:3**
**BWANA si mwepesi wa hasira , ana uweza mwingi; wala hatamhesabia mtu mwovu kuwa hatia kamwe; BWANA ana njia yake katika kisulisuli, na tufani, na mawingu ni mavumbi ya miguu yake.**

---

Asili ya Mkristo wa kweli ni kuwa mwepesi wa kusamehe, kupenda hata watu wasiostahili kabisa kwa sababu ya upendo ambao tulionyeshwa kwa mara ya kwanza kupitia Yesu Kristo msalabani. Ingawa hii ndiyo hali halisi ya kila Mkristo, watu wengi huchukulia mwenendo huu wa Ki-Mungu na kuulinganisha na kuwa wazembe na wasio na ulinzi mbele ya mashambulizi ya adui. Lakini hii haiwezi kuwa zaidi ya ukweli!

Mstari wa leo unatuambia kwamba Mungu hatawaacha wale wanaopigana nawe bila kuadhibiwa. Unapoweka mizigo yako kwa Hakimu wa ulimwengu, tumaini Yeye atatoa uamuzi unaolingana na makosa ambayo adui alitenda dhidi yako. Unamtumikia Mungu aliye mkuu katika uwezo. Usijali kuhusu kile ambacho mwanadamu anaweza kukufanyia, Yeye atalipa kila kosa ulilotendwa!

**TAMKO LA KINABII**
Ninamtumikia MUNGU WA HAKI! Kila tendo la uovu lililopangwa dhidi yangu na shetani halitapita bila kutambuliwa. Adui yangu ana HATIA KAMA ANAVYOSHITAKIWA! Mimi ni MSHINDI!

**MAFUNZO ZAIDI**
Kumbukumbu la Torati 32:4

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 74**
Kumbukumbu la Torati 4-6; Marko 10:1-31

JUMATATU, MACHI 16




# WODI TUPU ZA HOSPITALI

**Isaya 53:5**
**Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake; na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.**

---

Kama mtoto wa Mungu, afya ya Ki-Ungu ni haki yako kupitia upatanisho ambao Kristo alikuwekea kwa ufufuo Wake. Maisha ya kuumwa, magonjwa, na kutembelea hospitali kamwe hayakuwa sehemu ya mpango wa Mungu. Kataa kila mpango wa shetani kuleta magonjwa katika maisha yako na maisha ya familia yako, Kristo alikulipia ili uwe na afya kamilifu!

Unapotembea katika ukweli huu, Mungu anakuita kuwa mbebaji na msambazaji wa nguvu hizo hizo za uponyaji kwa wale wanaohitaji. Mungu amekupa mamlaka juu ya kila maradhi. Ni wajibu wako kuwaponya wagonjwa na kuwatoa katika giza na kuwaingiza katika nuru tukufu ya Mungu, mpaka kila chumba cha dharura, hospitali, na vituo vya kuwezesha kuishi maisha ya kawaida kiwe tupu!

**TAMKO LA KINABII**
Mungu amenipa maisha ya afya ya Ki-Ungu! Amenipa uwezo wa kusambaza nguvu hiyo hiyo ya uponyaji kwa wale wanaohitaji! Magonjwa na maradhi ni hali isiyo ya kawaida katika familia yangu, katika Jina la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Marko 16:17–18

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 75**
Andiko lako la leo: Kumbukumbu la Torati 7-9; Marko 10:32-52

**JUMANNE, MACHI 17**




# GPS YA MUNGU

**Wafilipi 1:6**
**Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu.**

---

Global Positioning System (GPS) hutumia mawimbi ya setilaiti ili kubainisha eneo lako kamili na kukuongoza kuelekea unakoenda. Moja ya vipengele vyake vya ajabu ni uwezo wake wa kukuelekeza. Haijalishi ni michepuko mingapi isiyo sahihi uliyoifanya, inakurudisha kwenye njia ya kuelekea mwisho unakoishia.

Kwa Mkristo, Mungu hufanya kazi vivyo hivyo. Bila kujali makosa au michepuko mibaya ambayo umiefanya, Yeye huendelea kufanya kazi ili kukurudisha kwenye njia kuelekea kile ambacho Kristo amekuitia kuwa. Usijielezee kulingana na maisha yako ya zamani. Mungu hajali makosa yako; Amejitolea kukurejesha na kukuelekeza kwenye njia sahihi kila hatua unayopitia.

**TAMKO LA KINABII**
Mafanikio yanahakikishiwa ninapofuata njia ambayo Kristo ameniwekea. Haijalishi maoni yangu mabaya hapo awali, nina hakika kwamba kazi njema ambayo Kristo ameanza ndani yangu, ataendeleza mpaka ikamilike katika Jina kuu la Yesu!

**MAFUNZO ZAIDI**
Yeremia 29:1

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 76**
Kumbukumbu la Torati 10-12; Marko 11

JUMATANO, MACHI 18




# JICHO LA DHORUBA

**Ufunuo 3:15-16**
**Nayajua matendo yako, ya kuwa hu baridi wala hu moto; ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu.**

---

Katika hali ya hewa, dhoruba kali kama vile vimbunga huundwa wakati hewa ya joto na baridi inapogongana, na hivyo kusababisha hali ya angahewa kutokuwa shwari. Hii huchochea upepo mkali, mvua kubwa, na mifumo fujo ya mgandamizo. Hata hivyo katikati ya yote kuna jicho la dhoruba, utulivu wa udanganyifu uliozingirwa na uharibifu.

Vivyo hivyo, kuwa moto na baridi kuhusu mambo ya Mungu huleta machafuko ya kiroho na kutokuwa na utulivu. Mtindo wa maisha ya nusu ndani, nusu nje unaweza kuonekana kuwa hauna madhara katikati, lakini huleta uharibifu kwa amani, kusudi na uhusiano wako na Mungu. Chagua leo kuweka mtazamo wako wote kwake. Kuwa na moto kamili kwa ajili ya Mungu, na utaona maajabu yake mengi yakifanyika katika maisha yako!

**TAMKO LA KINABII**
Ninakataa kuishi maisha ya uvuguvugu! Nimewekeza kikamilifu katika maisha ambayo Kristo amenipa. Kwa kuishi kwa ajili ya Mungu, ninaondoa dhoruba za bahati mbaya na uharibifu katika maisha yangu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Yakobo 1:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 77**
Kumbukumbu la Torati 13-15; Marko 12:1-27

ALHAMISI, MACHI 19




# NENO KATI YA WANYAMA WA MWITUNI

**Marko 1:13**
**Akawako huko jangwani siku arobaini hali akijaribiwa na shetani; naye alikuwa pamoja na wanyama wa mwitu, na malaika walikuwa wakimhudumia.**

---

Kujitenga kunatangulia kwanza na ndipo ufunuo! Kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, kujitenga ni muhimu kwa ajili ya kuondoa kila kikengeushacho, kikengeusha au vichepushaji. Takribani kila mhusika mkuu wa kibiblia alitumia muda akiwa peke yake kupokea maelekezo ya Mungu kabla ya kuingia katika udhihirisho kamili wa wito wake. Paulo alikaa miaka mitatu Arabuni, Musa miaka arobaini jangwani, na Yesu siku arobaini jangwani. Hii haikuwa bahati mbaya; kilikuwa chombo cha lazima ili kupatanisha masikio yao na Neno la Mungu.

Kujitenga kunamaanisha kunyamazisha kelele, hata wakati iko karibu nawe, na kueleekeza umakini wako kwenye kile ambacho Mungu anataka kuweka katika roho yako. Wakati wake wa kujitenga, Yesu alikabiliana na vikengeusha-fikira, kutoka kwa mashambulizi ya kishetani hadi hayawani-mwitu, na bado aliendelea kufokasi. Ilikuwa hapo, katika nguvu ya upinzani wa kiroho na wa kimwili, ambapo malaika walimhudumia.

**TAMKO LA KINABII**

Ninapochukua muda kumsikiliza Mungu, hata katikati ya hayawani-mwitu na vikengeusha-fikira, ninaimarishwa na kuhudumiwa!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 6:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 78**
Luka 5:1-19; Zaburi 29-31




# MZINGA WA NYUKI

**Mithali 13:20**
**Enenda pamoja na wenye hekima nawe atakuwa na hekima, bali rafiki wa wapumbavu ataumia.**

---

Mafanikio na maisha ya nyuki hutegemea manzuki aliyonayo. Katika mzinga, kila nyuki ana jukumu, wafanyakazi hukusanya nekta, wauguzi wanatunza watoto, walinzi wanalinda, na malkia hutaga mayai ili kuendeleza koloni. Ikiwa kundi moja litashindwa, usalama na utulivu wa mzinga uko hatarini. Vivyo hivyo, kama watoto wa Mungu, mara nyingi tunapuuza matokeo ya kuzungukwa na watu wasiofaa.

Fikiria kutembea kwako na Kristo kama mzinga wa kiroho unaoundwa na watu mbalimbali walio na nafasi ya kukusogeza kuelekea wito wako. Kuruhusu ushawishi mbaya kunaweza kuhatarisha ukuaji wako bila kukusudia na kuharibu mwelekeo wa maisha yako. Maandiko yanaonya kwamba ushirika wa wapumbavu unakupeleka kwenye uharibifu. Chagua kwa busara. Jizungushe na watu wenye nia moja ambao wana shauku ya kuendeleza Ufalme wa Mungu. Hatima yako ni ya thamani sana kuhatarisha miunganisho isiyofaa.

**TAMKO LA KINABII**
Ninatembea kwa hekima! Ninajitenga na kila ushawishi wa kijinga. Mahusiano yangu yanaonyesha kiwango cha mbinguni. Ninajilinganisha na watu wacha Mungu wenye kuendeshwa na fokasi, kama mimi!

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 15:33

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 79**
Kumbukumbu la Torati 16-18;
Marko 12:28-44

JUMAMOSI, MACHI 21




# MAPOKEO YA WANADAMU

**Marko 7:13**
**mkilitangua neno la Mungu kwa mapokeo yenu mliyopokeana...**

---

Mamilioni ya Wakristo wanateseka kwa sababu wanachukua maneno au desturi za wanadamu na kuzifanya kuwa mafundisho. Maandiko yanaonyesha wazi kwamba moja ya mambo machache yanayoweza kufanya Neno la Mungu lisiwe na ufanisi ni kuinuliwa kwa mapokeo ya wanadamu juu ya Neno la Mungu lisiloweza kukosea. Mwili unaotumia Duniani ni ganda tu, wewe halisi ni roho. Hii ina maana kwamba utamaduni wa nchi, jiji, na familia yako uko chini ya mamlaka ya juu ya Neno la Mungu.

Ikiwa utamaduni wa kilimwengu unahamasisha umaskini, uchungu, huzuni, au mawazo yoyote yanayopingana na viwango vya Mungu, yakatae. Mifumo kama hii inalenga kukuibia baraka na uhalisi wa kiroho uliofunuliwa katika maandiko. Mara tu ulipompokea Kristo, ulizaliwa upya katika utamaduni wa ubora na utawala juu ya mambo ya kidunia na ya kiroho. Tembea katika ubora huo leo!

**TAMKO LA KINABII**
Ninakataa desturi za ulimwengu huu! Kila imani au tamaduni ambayo haikukita mizizi katika maandiko haina nguvu kwangu. Neno la Mungu ndilo mamlaka ya mwisho katika maisha yangu; Ninatembea katika utimilifu wake leo!

**MAFUNZO ZAIDI**
Wakolosai 2:8

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 80**
Kumbukumbu la Torati 19-21;
Marko 13:1-20




# MWIZI WA FURAHA

**Isaya 60:22**
**Mdogo atakuwa elfu, na myonge atakuwa taifa hodari; Mimi, Bwana, nitayahimiza haya.**

---

Kuna msemo unasema, “Kulinganisha ni mwizi wa furaha.” Sentensi hii rahisi inaonyesha ukweli wa kina wa kibiblia. Wakristo wengi hupoteza amani na shangwe zao kwa kulinganisha hali zao za muda za kifedha, za ndoa, au za kitaaluma na za wengine. Maandiko yanatuhakikishia kwamba Mungu anatamani na anakusudia kutoa yaliyo bora tu kwa ajili yetu. Kama Baba mwenye hekima na ujuzi wote, Anajua wakati bora zaidi, njia, na majira ya kuachilia baraka hizo.

Mapambano haimaanishi kwamba Mungu amekuacha, wala haimaanishi kwamba siku kubwa zaidi hazijafika. Kamwe usifananishe maisha yako na kushindwa. Wengine wanaweza kuonekana mbele zaidi, lakini si wenye mbio washindao mbio. Mungu ana mpango kamili, wa kipekee kwa maisha yako, uliojaa baraka zilizohakikishwa!

**TAMKO LA KINABII**
Sifananishi maisha yangu na maisha ya wengine! Najua Mungu ana mpango wa kipekee na maalum kwangu. Sitaaibika au kufadhaika kamwe; Ninamtumikia Mungu anayefanya mambo YATOKEE! Haleluya!

**MAFUNZO ZAIDI**
Mhubiri 9:11

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 81**
Kumbukumbu la Torati 22-24;
Marko 13:21-37

JUMATATU, MACHI 23



# KUWAONEA WIVU WASIO MCHA MUNGU

**Zaburi 37:1-2**
**Usikasirike kwa sababu ya watenda mabaya, usiwahusudu wafanyao ubatili; maana kama majani watakatika mara, kama miche mibichi watanyauka.**

---

Wengi wanaishi chini ya fikira potofu kwamba Kanisa liko nyuma ya ulimwengu kijamii, na kuwafanya kuwahusudu wale walio na vyeo vya juu katika ufalme wa giza. Hata hivyo, maandiko yako wazi. Mtu anaweza kuwa na mali nyingi na ushawishi, lakini unapojua wewe ni nani na wa nani, hadhi ya mtu yeyote inafifia ukilinganishwa nae.

Kwa kuwastaajabia wasiomcha Mungu, unajifungulia mlango mwenyewe kuwa chini ya ushawishi wao na, kwa kuongezea, na wa Shetani, ukichukua hatua kwa hatua mazoea ya kilimwengu badala ya uadilifu. Katika Kristo, una mali, hadhi, na mamlaka kuu zaidi kuliko mtu yeyote aliye na giza. Hujafunzwa bora zaidi tu;  bali pia umeandaliwa mara elfu zaidi na kuwezeshwa kushinda kila changamoto ambayo adui analeta.

**TAMKO LA KINABII**
Ninakataa kuonea wivu mtindo wa maisha wa watu wasiomcha Mungu! Sitawahi kujiweka kwenye ushawishi wa adui. Haijalishi uwezo ambao wale wa ulimwengu wanaweza kushikilia, ninamtumikia Mungu ambaye ni mkubwa na mkuu kuliko wote! Bwana asifiwe. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 4:4

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 82**
Kumbukumbu la Torati 25-27;
Marko 14:1-36

JUMANNE, MACHI 24




# YOTE NI JUU YAKO

**Yakobo 1:22**
**Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidangaya nafsi zenu**

---

Je, unajua kiwango chako cha maisha, hasa kuhusu ustawi na afya, ni juu yako kabisa? Haijalishi wewe ni mwaminifu au umejitoa kiasi gani kwa Mungu, hatakupa tu afya au mali. Hizi si thawabu, ni matokeo ya kulitumia Neno Lake.

Mungu amekupa Neno lake kwa matarajio kwamba, kupitia utekelezaji wake, kila ahadi aliyotoa itadhihirika katika maisha yako. Hata hivyo, Wakristo wengi, bila kujua kanuni hiyo, wanakubali imani potofu kwamba "sikuzote mambo mabaya huwapata watu wazuri."

Ukweli ni kwamba, ingawa kujitolea kwa mtu kwa Mungu kuna thamani, hakuamui ubora wa uzoefu wa mtu wa Kikristo. Matumizi ya kanuni za maandiko hufanya hivyo. Mungu tayari amekupa uwezo na mamlaka ya kubadilisha maisha yako. Swali la kweli ni je, utaitumia?

**TAMKO LA KINABII**

Mafanikio yangu yote ni juu yangu! Mungu tayari amenipa rasilimali ili nifanikiwe. Mwaka huu, nitatumia yote aliyonipa kwa Jina kuu la Yesu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 10:19

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 83**
Kumbukumbu la Torati 28-29;
Marko 14:37-72

**JUMATANO, MACHI 25**



# UNACHOKIONA NDICHO UNACHOPATA

**Yoshua 6:2**
**BWANA akamwambia Yoshua, Tazama, nimeutia Yeriko katika mkono wako, na mfalme wake, na mashujaa wake.**

---

Ulimwengu wa kimwili unatawaliwa na kile kinachofanyika katika roho. Kwa hiyo, kabla ya kumiliki kile ambacho Kristo amekupa, ni lazima kwanza ukione kinadhihirika kiroho, si kuona kwa macho ya asili, bali kwa macho ya roho. Hii ni mojawapo ya kanuni zinazotawala za Ufalme.

Katika mstari wa leo, Yoshua anasimulia matukio yaliyotangulia vita vya Yeriko. Kabla ya jeshi lolote kukusanywa au silaha yoyote kuvutwa, Mungu alitangaza kwamba mji ulikuwa tayari umetiwa mikononi mwake. Yoshua alichohitaji kufanya ni kuona kwanza.

Mungu ameachilia yote unayohitaji ili kufanikiwa na kustawi. Lione likidhihirishwa katika ulimwengu wa kiroho kupitia maombi na kusoma Neno Lake, na hakika litachukua sura katika hali ya asili.

**TAMKO LA KINABII**
Ninaona ustawi, afya ya Ki-Ungu, madirisha ya fursa, na baraka zimewekwa mkononi mwangu! Tayari nimeshinda vita dhidi ya adui katika kila eneo la maisha yangu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Mwanzo 13:14–15

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 84**
Kumbukumbu la Torati 30-31;
Marko 15:1-24

ALHAMISI, MACHI 26




# MUNGU ANASEMAJE?

**Ayubu 22:28**
**Nawe utakusudia neno, nalo litathibitika kwako, na mwanga utaziangazia njia zako.**

---

Wakristo wengi wamepotosha maana ya kweli na umuhimu wa kile Maandiko hufundisha kuhusu nguvu ya kauli. Kukiri sio tu kubaki chanya au kuepuka hasi, ni juu ya kuweka maneno yako sawa na ukweli wa Neno la Mungu. Mstari wa leo unatukumbusha kwamba tunapoamuru kwa kupatana na Neno la Mungu, tunafanya mapenzi yake katika ulimwengu wa asili.

Kukiri si kuhusu kurudia-rudia bila akili kama kasuku. Ina nguvu pale tu maneno yako yanapoakisi kile ambacho Mungu anasema kukuhusu. Kwa hiyo, Yeye anasema nini? Anasema alikuja ili ufanikiwe na kuwa na afya njema. Kwamba una mamlaka juu ya falme na mamlaka. Kwamba wewe si wa ulimwengu huu. Tangaza kwa ujasiri! Si kweli tu kiroho; ni kweli kwako katika ulimwengu wa kimwili pia.

**TAMKO LA KINABII**
Maneno ninayozungumza yanapatana kabisa na Neno la Mungu. Ninapokiri kile ambacho Maandiko yanasema juu ya maisha yangu, ninasababisha ukweli huo kudhihirika kimwili, katika Jina la Yesu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 4:13

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 85**
Kumbukumbu la Torati 32-34;
Marko 15:25-47




# URAHISI DHIDI YA USADIKISHO

**2 Timotheo 4:2**
**Lihubiri neno; uwe tayari wakati ukufaao, na wakati usiokufaa; karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.**

---

Katika siku hizi za mwisho, wahudumu ulimwenguni pote hukazia umaana muhimu wa kuvuna nafsi kwa kuwatoa watu gizani na kuwaingiza katika nuru ya Mwana mpendwa wa Mungu, Yesu Kristo. Hata hivyo, Wakristo wengi hushiriki Injili tu wanapojisikia kuwa rahisi, badala ya wakati Roho Mtakatifu anapowahimiza kufanya hivyo. Mstari wa leo unatukumbusha kuwa ni wajibu wetu kuwa tayari kushiriki imani yetu, ndani na nje ya msimu.

Mungu hafanyi kazi kulingana na ratiba tunayopendelea. Roho Mtakatifu anapokuhimiza kunena, usingoje hadi wakati utakapojisikia sawa, tenda! Yesu, mfano wetu mkamilifu, alinena Neno kwa ujasiri, bila kujali wale waliomtakia mabaya. Kataa kutoafikiana na kile ambacho Maandiko yanaweka wazi. Usipuuze msukumo wa Roho kumfikia mtu fulani kwa injili. Chagua msukumo badala ya urahisi.

**TAMKO LA KINABII**
Daima niko tayari kueneza ujumbe wa Yesu Kristo kwa mtu yeyote, mahali popote, wakati wowote! Hofu ya kukataliwa haitazuia kamwe usadikisho wangu wa kuwasaidia wengine. Kama Yesu, ninachagua usadikisho badala ya urahisi! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 3:15

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 86**
Yoshua 1-3; Marko 16

JUMAMOSI, MACHI 28




# JUU YA HALI ZOTE

**Warumi 12:2**
**Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.**

---

Kuna ulimwengu zaidi ya asili hii, ulimwengu wa utukufu ambapo Neno la Mungu ni msingi mkuu. Katika ukweli huu wa hali ya juu, sheria pekee zinazofanya kazi zinatoka kwenye Neno la Mungu. Kupitia Kristo, wewe sasa ni wa ulimwengu huo, na Mungu amekupa Neno Lake ili kukufundisha maisha juu ya hali za kidunia. Kwa hivyo, usiseme kamwe, “Niko chini ya hali”, hiyo haiwezi kamwe kuwa ukweli wako. Katika Kristo, unaishi juu ya kila hali mbaya.

Ili kutembea kikamilifu katika hali hii ya juu zaidi, akili yako lazima inyenyekee Neno la Mungu kila siku. Kwa kuuweka mwili wako chini ya ukweli wa Ki-Ungu wa Mungu, unajiweka huru kutoka kwenye mifumo ya ulimwengu ya magonjwa, ukosefu, huzuni na bahati mbaya, na kuingia katika ukweli wako mpya wa utele na kustawi.

**TAMKO LA KINABII**
Ninaishi juu ya hali zote! Ninaishi maisha yaliyo mbali na matatizo ambayo ulimwengu unakabili. Nilizaliwa katika ulimwengu wa utukufu wa Mungu! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 2:6

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 87**
Yoshua 4-6; Yohana 1:1-28

JUMAPILI, MACHI 29



# KAMA BABA, KAMA MWANA

**2 Wakorintho 3:18**
**Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.**

---

Bwana Yesu aliishi duniani si kama Mwana wa Mungu katika ukuu Wake kamili, bali kama Mwana wa Adamu. Alichagua kufanya kazi kama mwanadamu ili kuonyesha kwamba miujiza, ishara, na maajabu Aliyofanya yanaweza pia kufanywa na wewe, mtoto Wake, hata ukiwa katika mwili huu wa duniani.

Unaposoma Injili na kushuhudia shuhuda zenye nguvu za huduma Yake, usione kazi Zake kuwa haziwezi kufikiwa. Kristo alikuja kuwa mfano kamili, mwongozo wa jinsi tunavyokusudiwa kuishi. Kifo chake msalabani hakikuwa tu kwa ajili ya ukombozi; ilikuwa ili upate na kuenenda katika nguvu na uzima uleule alio nao.

**TAMKO LA KINABII**
Nina uzima wa Kristo ndani yangu! Bwana Yesu ndiye kielelezo changu kikamilifu, na ninaposoma na kutafakari Neno Lake, ninabadilishwa kila siku kuwa sura yake. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 4:17

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 88**
Yoshua 7-9; Yohana 1:29-51

**JUMATATU, MACHI 30**



# KITAKACHOKUWA, KITAKUWA

**Luka 10:19**
**Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.**

---

Kuna janga la Wakristo ambao wanashindwa kutambua uwezo wao wa kubadilisha hali zao. Wengi huitikia maisha kwa urahisi, wakiruhusu hali kuamuru matokeo yao, badala ya kufanya mabadiliko. Kauli kama vile “Kitakachokuwa, kitakuwa” au “Ikiwa ni yangu, itanijia” ni uwongo kutoka kwa adui ulioundwa kuzuia urithi wako.

Kama mtu aliyezaliwa na Mungu, umepewa mamlaka na uwezo wa kupindua kila mpango na mawazo mabaya ya adui. Unaweza kuita yawepo yote ambayo Kristo amekupa. Hii ina maana unaweza kutangaza mafanikio yako, afya ya Ki-Ungu, na kuamuru kila aina ya baraka kuja kwa kasi katika maisha yako. Shika Neno la Mungu leo, tembea katika uhalisi wake, na ushuhudie maisha yako yakibadilika milele.

**TAMKO LA KINABII**
Siwezi kufumbwa macho kamwe! Hakuna hali iliyo nje ya uwezo wangu wa kubadilika. Mimi si Mkristo ninayelipuka; Ninasababisha mambo kulipuka! Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Wafilipi 4:13

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 89**
Yoshua 10-12; Yohana 2

JUMANNE, MACHI 31




# UJINGA WA NENO

**Hosea 4:6**
**Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako.**

---

Katika mahakama ya sheria, ujinga kamwe si kisingizio halali. Cha kusikitisha ni kwamba, Wakristo wengi hawajui ukweli wa maandiko. Kwa hiyo, wanaishi maisha ya kawaida yanayokumbwa na maumivu, umaskini, ukosefu, na mapambano. Si kwa sababu ni mapenzi ya Mungu, bali kwa sababu hawajui kilicho haki yao.

Biblia iko wazi: Watu wa Mungu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa, si kwa sababu adui ana nguvu nyingi sana, bali kwa sababu hawana vifaa vya kumpinga. Neno la Mungu ni ghala yako ya silaha. Kwa kulisoma na kulitafakari, unapata silaha za kiroho za kushinda kila shambulio la shetani. Kataa kuishi chini ya kiwngo cha urithi wako. Tembea katika nguvu na ahadi za Neno la Mungu!

**TAMKO LA KINABII**
Mimi ni Mkristo ninayesoma! Kupitia kusoma Neno la Mungu, ninajitayarisha kwa vita. Ninaposoma Neno, adui hana nafasi! Utukufu ni kwa Mungu. Amina.

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 5:13

**MKAKATI WA KUSOMA BIBLIA WA SIKU 365 – DAY 90**
Yoshua 13-15; Yohana 3:1-21




# MWONGOZO WAKO WA KINABII WA KILA SIKU

Gazeti la Habari Njema Kila Siku linafurahi kutambulisha matoleo mahususi yaliyoundwa kwa uangalifu kwa ajili ya vijana na watoto, yakiandamana na ibada yetu kuu. Kila toleo hutoa Neno la kinabii la kila siku moja kwa moja kutoka moyoni mwa Nabii Uebert Angel, lililowasilishwa kwa njia ambayo inazungumza na kila hatua ya maisha na kuunganishwa na kila mwanafamilia.

Ibada hizi zimewekwa pamoja kwa uangalifu ili kufanya Neno la Mungu liwe hai kwa njia inayohusiana na yenye matokeo, kusaidia wasomaji kukua katika imani, ufahamu na ukomavu wa kiroho. Dhamira yetu ni kuhakikisha kwamba ukweli wa Mungu unafikia mioyo ya vizazi vyote, na kutia moyo kutembea Naye kwa kina kila siku.




**TOLEO LA VIJANA**

Huingia ndani zaidi na maarifa yenye nguvu ambayo huwapa vijana kukabiliana na changamoto za maisha kwa hekima na nguvu za kiroho.

**TOLEO LA WATOTO**

Imeundwa ili kutambulisha dhana za msingi za imani, upendo, na ahadi za Mungu kwa njia ya kufurahisha na ya kuvutia ikisaidia mioyo michanga kusitawisha uhusiano thabiti na Mungu na kuifanya Biblia iwe hai.

Kila siku, utapokea Neno lako la Kinabii la Siku lililoandikwa na Nabii Uebert Angel, ujumbe wa kiungu wa kuimarisha kutembea kwako na Mungu na kukuongoza katika kuishi kwa Neno lake. Ni njia yenye nguvu kwa familia kukua pamoja katika imani na kuimarisha uelewa wao wa ukweli wa Mungu.

## USIKOSE!

Anza kufurahia nguvu ya mabadiliko ya GoodNews Daily, mwongozo wa kinabii ulioundwa kuinua na kutia moyo kila kizazi!

SCAN ME



BWANA WETU

# YESU KRISTO

Bwana wetu Yesu Kristo ndiye msingi wa imani ya Kikristo, maisha yake na mafundisho yake yameathiri sana mwendo wa historia. Bwana wetu Yesu Kristo anajulikana kwa huruma yake isiyo na kifani, hekima, na matendo ya miujiza Aliyofanya. Ujumbe wake ulijikita katika upendo, msamaha, na ahadi ya uzima wa milele, ukitoa tumaini na ukombozi kwa wote wanaomwamini. Katika huduma Yake yote, Alisafiri katika nchi za Yudea, akiponya wagonjwa, akiwafariji walioteseka, na kufundisha kuhusu ufalme wa milele wa Mungu.

Kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako binafsi kunamaanisha kukubali mafundisho Yake na kualika uwepo Wake wa mabadiliko maishani mwako. Ni safari ya kuelekea utimilifu wa kiroho, yenye msingi katika imani, upendo, na ahadi ya wokovu.

Kupitia Bwana wetu Yesu Kristo, tunapata nguvu, tumaini, na njia ya amani ya milele. Kufanywa kuwa mkamilifu, au kuokolewa, ni kujisalimisha kwa Mungu na mpango wake na kusudi lake kwa maisha yetu. Ni kugeuka kutoka kwenye njia zetu za zamani na kumgeukia Yesu Kristo, kumwomba msamaha kutoka kwenye dhambi zetu na kutupa maisha mapya ndani yake.

**WARUMI 10:9**
**"Ukikiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka."**

Wokovu ni zawadi ya bure ya Mungu kwetu na tunakuwa watoto Wake. Ni kibali kisichoweza kubatilishwa katika familia ya Mungu na ni uwezeshaji wa kuishi maisha kikamilifu na kikamilifu kwa kusudi la kumwakisi Mungu kwa uumbaji Wake wote.



### JE, UMEMPOKEA

# YESU KRISTO?

**“Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.” - Luka 19:10**

**TUNAWAKARIBISHA KUMFANYA YESU KRISTO, BWANA WA MAISHA YAKO KWA KUOMBA SALA HII:**

“Ee Bwana Mungu, ninakuja kwako katika jina la Yesu Kristo. Ninaamini kwa moyo wangu wote katika Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Ninaamini kwamba alikufa kwa ajili yangu na Mungu alimfufua kutoka kwa wafu. Ninaamini yu hai leo. Ninakiri kwa kinywa changu kwamba Yesu Kristo ndiye Bwana wa maisha yangu tangu siku hii. Kupitia Yeye na kwa jina Lake, nina uzima wa milele; nimezaliwa mara ya pili.”

Asante Bwana, kwa kuokoa roho yangu!
Sasa mimi ni mtoto wa Mungu. Haleluya!”

**Hongera! Sasa wewe ni mtoto wa Mungu.**

**Endelea kukua kwa kukaa katika Neno Lake, kuomba kila siku, na kuweka imani yako kuwa imara. Mungu ana safari ya ajabu mbele yako.**

**Ili kukua zaidi kama Mkristo wasiliana nasi:**
**UK:** +44 3333 448 612 | **USA** +1 240 781 6942
**RSA:** +27 51 004 0209 | **ZWE** +263 773 195 955
**Email: gnd@goodnewsworld.com**

SCAN ME



**KIFUNGU CHA MAANDIKO YA**

# ULINZI

**Umezungukwa na Nguvu za Mungu, Hakuna Ubaya Unaoweza Kusimama Juu Yako!**

**ISAYA 54.**

**14.** Nimejenga imara, niliyowekwa katika haki. Mbali na shida yoyote, hakuna cha kuogopa! Mbali na hofu, hata haitakuja karibu!

**15.** Mtu akinishambulia, sitafikiri hata kidogo kuwa Mungu ndiye aliyemtuma. Na ikiwa yeyote atanishambulia, hakuna kitakachotokea.

**16.** Mungu alimuumba mhunzi ateketeze mfua chuma chake na kutengeneza silaha iliyoundwa kuua. Pia amemuumba mharibifu.

**17.** Lakini hakuna silaha inayoweza kunidhuru iliyowahi kughushiwa. Yeyote anayenituhumu ataondolewa kuwa mwongo. Mimi ni mtumishi wa Mungu hivyo ndivyo ninavyoweza kutarajia Mungu atahakikisha kwamba kila kitu kinaenda vyema kwa ajili yangu.

**Hivi ndivyo Mungu anasema na haitashindwa katika jina la Yesu!**

**Ili kukua zaidi kama Mkristo wasiliana nasi:**
**UK:** +44 3333 448 612 | **USA** +1 240 781 6942
**RSA:** +27 51 004 0209 | **ZWE** +263 773 195 955
**Email: gnd@goodnewsworld.com**

SCAN ME



# KARAMA YA WOKOVU

**WARUMI 10:9**
**"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.**

Wokovu ni muujiza mkuu kuliko yote. Haipatikani kwa matendo mema au jitihada za kidini, ni zawadi ya bure kutoka kwa Mungu. Yesu Kristo alipokufa na kufufuka tena, alifungua njia kwa kila mtu kuokolewa kutoka kwa dhambi na kuletwa katika uzima wa milele. Mikono yake imefunguliwa kwa upana, tayari kumkaribisha yeyote anayeamini na kuliitia jina Lake.

Haijalishi umekuwa wapi au umefanya nini. Damu ya Yesu inaosha kila dhambi, kila kosa na kila kushindwa. Katika dakika moja ya imani, maisha yako ya nyuma yanafutwa, na maisha mapya kabisa huanza. Unachotakiwa kufanya ni kuamini moyoni mwako kwamba Yesu ni Bwana na umkiri kwa kinywa chako. Sasa hivi, unaweza kumpokea.



Sema: **"Bwana Yesu, ninaamini ulikufa kwa ajili yangu na ukafufuka. Ninakupokea kama Bwana na Mwokozi wangu."**

**Hivyo ndivyo ilivyo, umezaliwa mara ya pili! Umepita kutoka mautini kuingia uzimani.**



# WAKATI WA KUPONYA KWAKO

**1 PETRO 2:24**
**"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; ambaye kwa kupigwa kwake mliponywa."**

Uponyaji sio ahadi inayongojea kutokea; ni kazi iliyokamilika. Yesu aliponing'inia kwenye msalaba huo, hakubeba dhambi zako tu, alibeba kila ugonjwa, kila maumivu, na kila udhaifu. Mapigo ya mgongo Wake yalikuwa malipo ya utimilifu wako.



Huhitaji kuhangaika kupata uponyaji; uponyaji wako ulilindwa zaidi ya miaka elfu mbili iliyopita. Sasa, kilichobaki ni wewe kuamini. Mara tu unapomkubali Yesu Kristo, nguvu iyo hiyo iliyomfufua kutoka kwa wafu huanza kufanya kazi katika mwili wako.

**Speak life to every cell and every bone. Refuse to see yourself as sick. Instead, declare with boldness:**

**"Kwa kupigwa Kwake, mimi nimeponywa."**

Hivi sasa, nguvu hiyo ya uponyaji inapita ndani yako. Kila dalili lazima iliinamie jina la Yesu.

**Pokea, uponyaji wako umefika.**

GoodNews DAILY



# DIRA YA DUNIA INAHITAJI BAJETI YA ULIMWENGU

**KUWA MPENZI WA GOODNEWS KILA SIKU**



Kila mwezi, washirika wetu waliojitolea husambaza nakala za ibada ya GoodNews Daily bila malipo kwa watu katika vituo vya watoto yatima, magereza, hospitali, nyumba za wazee, shule, taasisi za serikali na maeneo mengine mengi duniani kote. Tumepokea shuhuda nyingi za wokovu, uponyaji, utoaji wa kimungu, na miujiza mingine mingi kama matokeo ya kampeni hii ya kimataifa ya usambazaji.

Jiunge nasi na uwe sehemu ya harakati hii tukufu ya Mungu, ukimpa mtu mabadiliko ya mwanzo mpya na matumaini mapya ya kesho.

**To further grow as a Christian contact us:**
**UK:** +44 3333 448 612 | **USA** +1 240 781 6942
**RSA:** +27 51 004 0209 | **ZWE** +263 773 195 955
**Email: gnd@goodnewsworld.com**

SCAN ME




### UJUMBE MMOJA

# LUGHA NYINGI

**KWA SABABU UJUMBE WA KRISTO HAUJUI KIZUIZI CHA LUGHA**

Gazeti la Habari Njema Kila siku linabadilisha maisha duniani kote kupitia tafsiri katika lugha nyingi zinazozungumzwa na watu wengi, na hivyo kuwapa mamilioni ya watu uwezo wa kupata maarifa ya kuokoa ya Yesu Kristo. Kote katika mataifa na tamaduni, watu kila mahali wanakutana na Neno la kinabii na kupata uzoefu wa kubadilisha maisha na Mungu kupitia ibada hii.




Gazeti la Habari Njema KIla siku linavunja vizuizi na kuzungumza moja kwa moja ndani ya mioyo ya watu katika lugha yao wenyewe. Kuanzia majumbani na shuleni hadi makanisani, vyuo vikuu na hata miongoni mwa viongozi na marais, inafikia kila ngazi ya jamii.

Kwa kubeba Neno la kinabii la Nabii Uebert Angel kwa kila taifa na kila lugha, GoodNews Daily inasaidia kutimiza Agizo Kuu katika kizazi hiki.

**ILI KUDHAMINI TEMBELEA TOVUTI YETU:**

www.goodnewsdailydevotional.com

**KARIBU**

# MTANDAONI KWETU



**KUJUA ZAIDI TEMBELEA TOVUTI YETU LEO**

Tembelea tovuti ya GoodNews Daily ili kupata ibada za watu wazima, vijana, na watoto, kila moja iliyoandikwa kwa uangalifu ili kuimarisha imani yako na kuongeza uelewa wako wa Neno la Mungu. Tovuti hii pia ina mafundisho ya utambuzi kutoka kwa Nabii Uebert Angel, masasisho kuhusu matukio ya hivi punde ya GoodNews Daily, na nyenzo mbalimbali zilizoundwa kukusaidia kukua na kustawi katika kila eneo la maisha yako.

Iwe unatafuta maongozi ya kila siku, ufunuo wa kina, au njia za kuendelea kuwasiliana na Ulimwengu wa Habari Njema, kila kitu unachohitaji kinapatikana katika sehemu moja kwenye tovuti ya GoodNews Daily.

**Ungana nasi kwenye mitandao ya kijamii:**
@goodnewsdailydevotional




## KILA SIKU

Spotify

Jiunge na jumuiya yetu ya wasikilizaji wa kimataifa ambao huanza siku kwa habari njema kilasiku. Sikiliza Habari Njema kwenye Spotify na uambatane nayo kwenye ukuaji wa kiroho na ukweli wa kibiblia chini ya ufunuo na mafundisho ya Nabii Uebert Angel.



## KILA SIKU

Youtube

Tunakuletea shuhuda za maisha halisi kuhusu matokeo ya Habari Njema Kila Siku ibada imekuwa duniani kote kupitia chaneli yetu ya YouTube. Kama shajala nambari moja ya kila siku, imegusa maisha ya kutosha, ikieneza ujumbe wa tumaini, upendo na imani. Kupitia mafundisho mazito ya nabii Uebert Angel, shajala ya habari njema kila siku imekuwa chombo chenye nguvu cha kibinafsi cha mageuzi, kuhamasisha watu binafsi, familia, na watoto kuishi maisha yao kusudi na utimilifu.

Imeandikwa na Nabii Uebert Angel

SUBCRIBE NOW

@GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL

WWW.GOODNEWSDAILYDEVOTIONAL.COM

GoodNews DAILY

CONNECT

A FRESH WORD EVERYDAY, ONE TAP AWAY




**SASA INAPATIKANA**

Endelea kushikamana na Neno popote ulipo! Fikia jumbe za kila siku za ibada, zenye kutia moyo na mafundisho yenye nguvu kutoka kwa Nabii Uebert Angel ambayo yataimarisha na kujenga imani yako kila siku.

Get it on Google play

Available on the App Store

www.goodnewsdailydevotional.com

# DUKA LETU

## MAMBO MUHIMU YOTE KATIKA SEHEMU MOJA




**HABARI NJEMA KILA SIKU COMPENDIUM TOLEO YA KWANZA**

Kuishi maisha yenye matunda ndani ya Kristo huanza na hamu ya kujua na kuelewa Neno la Mungu. GoodNews Daily Compendium, iliyoandikwa na Prophet Uebert Angel, hurahisisha shughuli hii na kuwa na maana zaidi. Buku la 1 linaleta pamoja sura nyingi zenye nguvu zilizojaa ibada na mafundisho juu ya mada tofauti, zote zikiwa zimepangwa kwa njia ambayo ni rahisi kufuata na kuelewa. Kila ukurasa hukusaidia kuimarika katika imani, kupata umaizi wa kina katika Injili hii, na kupata uzoefu wa nguvu zinazobadilisha maisha za Neno la Mungu kila siku.

**TUMIA MSIMBO HAPA CHINI KWA PUNGUZO LA 10% UNUNUZI WA KWANZA:G O O D N E W S 1 0**

**CHEKI HAPA KWA DUKA KAMILI**

# TOLEO LA | 2026
## Januari - Februari - Machi

---

Habari Njema Kila Siku inatengenezwa na Spirit Embassy:
Kanisa la GoodNews, likishiriki mafundisho ya kinabii na ufunuo wa Nabii Uebert Angel. Imejitolea kueneza ujumbe wa Yesu Kristo na kuwatia nguvu waumini kwa Neno la Mungu.

**KWA HABARI ZAIDI, MAOMBI, AU ILI KUHUSISHWA, TAFADHALI WASILIANA NA TAWI LAKO**

Jina la Tawi:
Mtu wa Mawasiliano:
Nambari ya Simu:
Barua pepe:
Anwani:

**Hakimiliki © 2025 na Uebert Angel**
**Haki zote zimehifadhiwa.**

support@goodnewsworld.com
www.goodnewsworld.com

Kwa habari zaidi au kushiriki ushuhuda wako:
gnd@goodnewsworld.com | www.goodnewsdailydevotional.com

**Ili kukua zaidi kama Mkristo wasiliana nasi:**
**UK:** +44 3333 448 612 | **USA** +1 240 781 6942
**RSA:** +27 51 004 0209 | **ZWE** +263 773 195 955
**Email: gnd@goodnewsworld.com**

SCAN ME



For further information on how to grow as a Christian, please get in touch with us at:


UK: +44 3333 448 612
USA +1 240 781 6942
RSA +27 51 004 0209
ZWE +263 773 195 955

**gnd@goodnewsworld.com**
**goodnewsdailydevotional.com**


SCAN FOR YOUR FREE DOWNLOAD